# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI

*Dar es Salaam*
*10 Januari, 2025*

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### MAENDELEO YA UWEKEZAJI NA MABORESHO YA MAZINGIRA YA BIASHARA KWA MWAKA 2024 NA MWELEKEO KWA MWAKA 2025

1. Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, ilipoingia madarakani, pamoja na mambo mengine, ilidhamiria kukuza uwekezaji na kuboresha mazingira ya biashara kama sehemu ya mikakati muhimu ya kuchochea ukuaji wa uchumi nchini. Katika taarifa hii tunaeleza kwa muhtsari maendeleo ya sekta ya uwekezaji kwa mwaka 2024 na mwelekeo kwa mwaka 2025.

2. Mafanikio katika sekta ya uwekezaji hupimwa kwa kuzingatia vigezo vikubwa vitatu. Vigezo hivi ni **idadi ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa, idadi ya ajira zilizozalishwa kupitia miradi iliyosajiliwa**, na **mtaji uliovutiwa kutokana na miradi hiyo**. Majukumu ya kuhamasisha, kuwezesha na kuratibu utekelezaji wa miradi ya uwekezaji nchini husimamiwa na kuratibiwa na taasisi mbili za umma: Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Kusimamia Uzalishaji wa Bidhaa kwa Ajili ya Mauzo Nje ya Nchi (EPZA).


3. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2024, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kilisajili jumla ya **miradi 901**, ukilinganisha na miradi 526 iliyosajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Hii ni sawa na **ongezeko la asilimia 71.3 la miradi iliyosajiliwa katika kipindi cha mwaka mmoja**.

4. Miradi iliyosajiliwa mwaka jana (2024) inatarajiwa kuzalisha ajira 212,293 ukilinganisha na ajira 137,010 zilizozalishwa na miradi ya uwekezaji katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Aidha, miradi hii imeweza kuvutia mtaji wa dola za kimarekani bilioni 9.31, ukilinganisha na mtaji wa dola za Kimarekani bilioni 5.72 iliyotokana na miradi ya uwekezaji kupitia TIC katika kipindi cha Januari – Disemba 2023.

5. Mikoa mitano inayoongoza kwa kusajili miradi ya uwekezaji nchini ni ***Dar es Salaam*** (356), ***Pwani*** (166), ***Arusha*** (64), na ***Dodoma*** (47), ambapo asilimia 70.3 (miradi 633) ilisajiliwa katika mikoa hii.

6. Sekta tano zinazoongoza kwa kusajili miradi mingi ya uwekezaji ni ***uzalishaji viwandani*** (miradi 377, 41.8%), ***usafirishaji*** (miradi 138, 15.3%), ***ujenzi wa majengo ya biashara*** (miradi 91, 10.1%), ***utalii*** (miradi 76, 8.4%), na ***kilimo*** (66, 7.3%). Miradi katika sekta hizi kwa pamoja zilivutia jumla ya mtaji wa dola za Kimarekani bilioni 6.071, sawa na asilimia 65.2 ya mtaji wote uliopatikana kwa mwaka 2024.

7. Mwaka 2024 tunaweza kuutangaza kuwa ***mwaka bora zaidi katika sekta ya uwekezaji Tanzania*** kutokana na ukweli kwamba ndio mwaka ambao TIC ilisajili miradi mingi zaidi ya uwekezaji (miradi 901) tangu Tanzania ianzishe kituo hiki na kuanza kurekodi miradi ya uwekezaji kama inavyooneshwa katika umbo la hapa nchini. **Hii inavunja rekodi ya miradi 885 ya mwaka 2013**.




***Umbo*: Idadi ya Miradi Iliyosajiliwa Katika Kituo cha Uwekezaji 1996-2024**

8. Hadi kufikia Disemba 2024, TIC ina **miradi 13,282 ya uwekezaji** iliyosajiliwa na kutekelezwa nchini, ikivutia **mitaji kiasi cha dola za kimarekani 127,176 milioni** na kutoa ajira zaidi ta **1.98 milioni.**

9. Mafanikio katika sekta ya uwekezaji yamechochewa na sababu mbalimbali kama ifuatavyo:

   i) **Kuendelea kumiarisha mifumo ya kisera na sheria** katika kuwezesha na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini

   ii) **Maono, hamasa na ushawishi ambao umeendelea kufanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** kwa makampuni mbalimbali ya kimataifa kuja kuwekeza nchini kupitia ziara na mikutano mbalimbali aliyoifanya nje na ndani ya nchi

   iii) **Kampeni kubwa ya kitaifa ya kuhamasishaji uwekezaji nchini iliyofanyika mwaka jana kwa ushirikiano mkubwa katika ya TIC, chemba za biashara nchini (TCCIA, TWCC), Mabenki, na vyombo vya habari**. Jumla ya wafanyabiashara 1,800 walifikiwa kupitia kampeni hii katika mikoa 26 ya Tanzania Bara

   iv) **Kuendelea kuimarisha na kuboresha huduma kwa wawekezaji katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)** ambapo sasa kuna taasisi 16 zinazotoa huduma katika kituo cha pamoja

   v) **Kuanzishwa kwa ofisi mpya ya Kanda ya Kaskazini mkoani Arusha**

   vi) **Viongozi katika sekretariati za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa, hususan wakuu wa mikoa, kuendelea kuhamasisha shughuli za uchumi na uwekezaji katika maeneo yao**

10. Katika kuendelea kuimarisha sekta ya uwekezaji nchini na kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, **Serikali kwa mwaka 2025 itachukua hatua zifuatazo:**

i) **Kutunga Muswada wa Sheria Mpya ya Uwekezaji Tanzania. Pamoja na mambo mengine, muswada huu unapendekeza kuunganisha taasisi za TIC na EPZA.** Muswada huu uliwasilishwa Bungeni mwaka 2024 na sasa upo katika ngazi ya Kamati ya Kudumu ya Bunge kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

ii) **Kuandaa awamu ya pili ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI).** Hii ni baada ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa MKUMBI I uliobaini mafanikio mbalimbali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Aidha,tathmini hii ilibaini changamoto mpya zilizojitokeza ambazo serikali na wadau wanaendelea kuzifanyia kazi. Lengo ni kuifanya Tanzania kuwa moja ya nchi zenye mazingira bora ya kufanya biashara na uwekezaji barani Afrika.

iii) **Kuanzisha utaratibu wa kuzipima mamlaka za serikali za mitaa** katika kuboresha mazingira ya biashara na kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji

iv) **Kuanza kutekeleza ujenzi wa miundombinu katika maeneo maalum ya kiuchumi ikiwemo la Bagamoyo** (Bagamoyo Special Economic Zone) ili kuwezesha ujenzi wa viwanda.

v) **Kushirikiana na watanzania waishio nje ya nchi (diaspora) kuanzisha utaratibu wa kuhamasisha uwekezaji** kwa kuzingatia taratibu zitakazowekwa na TIC kwa kushirikiana na mamlaka zingine za serikali

vi) Kwa mwaka 2025, **tumejiwekea lengo la kuvutia miradi MIPYA 1,500 ya uwekezaji na mitaji ya dola za kimarekani 15 bilioni ifikapo Disemba 2025 ($15 billion).** Sekta mahsusi ni viwanda, kilimo, uchukuzi, nishati safi, utalii, madini na huduma (service sector)

**Ongezeko hili litaifanya Tanzania kuwa moja ya nchi 5 bora katika uwekezaji barani Afrika hasa kwa wingi wa mitaji.** Kwa utoaji wa huduma, Tanzania ni moja ya nchi bora kwa uwekezaji hata sasa.

vii) **Tutaendelea kuhamasisha uwekezaji wa ndani tukiwa na lengo la kufikisha 50% ya miradi yote ya uwekezaji kwa mwaka imilikiwe na watanzania.** Tutashirikiana na taasisi mbalimbali za serikali kuwalenga wawekezaji wa ndani hasa wawekezaji wadogo wanaokua.

viii) **Kuboresha na kuwezesha ofisi za Sekretariat za Mikoa katika kuhudumia na kuboresha mazingira ya uwekezaji** katika ngazi na Mikoa na Wilaya nchini kote. **Kwa mwaka 2025, tutaanza na kufungua ofisi ya Kanda ya TIC mkoani Njombe** ili kusogeza huduma za uwekezaji mkoani Njombe, Iringa na Ruvuma.

***Imetolewa na:***

Prof. Kitila Alexander Mkumbo **(Mb.),**

**WAZIRI WA NCHI,**
**OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI.**

**Dar Es Salaam, ijumaa 10 Disemba, 2025**

***Kwa mawasiliano na taarifa zaidi:***

**Raymond Mtani,**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini,
Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji,
S.L.P 104,
**DODOMA.**
**Simu: +255 (0) 767074991**
**Email:** raymond.mtani@planninginvestment.go.tz